**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**TAARIFA KWA UMMA**

# MPANGO WA UFADHILI WA KUJIENDELEZA KWA WATUMISHI WA UMMA KADA ZA AFYA KUPITIA *SAMIA HEALTH SUPER-SPECIALIZATION PROGRAM* KWA MWAKA 2025/2026

**Dodoma, 21 Agosti, 2025.**

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** imeendelea kufanya mageuzi makubwa ndani ya Sekta ya Afya, lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za matibabu hasa ya kibingwa na ubingwa bobezi hapa nchini.

Katika kufanikisha azma ya kuwa na watalaam wenye ujuzi wa kutosha wa kutoa huduma bora za matibabu hapa nchini, Wizara ya Afya ilijiwekea lengo la kusomesha wataalamu bingwa na bobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha kupitia Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Serikali unaojulikana kama '***Samia Health Super-Specialization Program***'. Jitihada hizo zinalenga kuimarisha na kusogeza huduma bora za afya, kupunguza rufaa za matibabu nje ya nchi na hivyo kupunguza gharama kwa Serikali na wananchi pamoja na kuvutia tiba utalii.

***Samia Health Super-Specialisation*** *Program* ni mpango maalum wa kutoa ufadhili wa masomo ya ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi unaosimamiwa na Wizara ya Afya kwa ajili ya kuwaendeleza watumishi wa Sekta ya Afya kusoma masomo ya kibingwa na kibobezi kwenye fani mbalimbali za afya zinazotolewa kwenye vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kupitia ufadhili huu wanufaika wanalipiwa ada na posho ya utafiti kwa wanaosoma vyuo vya ndani ya nchi na kwa wanaosoma nje ya nchi wanalipiwa ada, nauli, posho ya utafiti na posho ya kujikimu. Malipo ya posho ya utafiti na posho ya kujikimu yatazingatia viwango vilivyopangwa na Wizara. Ufadhili huu **sio mkopo** ni ***grant*** wanayopewa wanufaika kwa masharti maalum ya kuendelea kufanya kazi nchini baada ya kuhitimu.

Programu hii inatoa ufadhili kwa mafunzo yanayotolewa kwa utaratibu wa kawaida wa mtumishi mmoja mmoja anayekwenda masomoni au kwa utaratibu wa **seti** ambapo watumishi wa fani mbalimbali wenye lengo la kuanzisha huduma ya kibingwa au kibobezi wanakwenda masomoni kwa pamoja kusoma taaluma husika ya kibobezi kwa kuzingatia eneo la utaalamu analopaswa kujengewa uwezo kila mwanataaluma.

Mfano, unapoanzisha huduma ya kusafisha figo (renal dialysis) katika hospitali, inakulazimu kusomesha wataalamu bingwa/bobezi wa figo wa kada za udaktari, uuguzi, famasi, maabara, mshauri nasaha, fiziotherapia pamoja na mtaalamu wa tiba kazi (occupational therapy) mwenye utaalamu wa kuhudumia wagonjwa wa figo.

Kwa mwaka huu wa fedha 2025/2026, Wizara imetengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 9** kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu katika ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi katika fani mbalimbali za kipaumbele katika Sekta ya Afya. Fedha hizi ni kwa ajili ya kugharamia mafunzo kwa wataalamu bingwa na bobezi watakaokuwa wanaendelea na masomo pamoja na wapya watakaopata ufadhili kwa mwaka 2025/2026.

Wizara inawatangazia wataalamu wote waliopata udahili wa masomo katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi kwa mwaka 2025/2026 kwamba dirisha la kutuma maombi ya ufadhili wa ***Samia Health Super-Specialization Program 2025/2026*** limefunguliwa kuanzia tarehe 20 Agosti, 2025 hadi tarehe 12 Septemba, 2025. Maombi ya ufadhili yawasilishwe kwa njia ya kielektroniki kupitia tovuti https://***esponsorship.moh.go.tz/*** Aidha, nasisitiza kuwa maombi yatakayofanyiwa kazi ni yale yatakayowasilishwa kwa njia ya mfumo huo tu.

Wizara imeweka vigezo vya ujumla pamoja na vigezo mahsusi vya kupata ufadhili huu ambavyo vimeainishwa kwa kina kwenye tangazo la ufadhili. Vigezo vya ujumla vitakavyotumika ni pamoja na mtumishi atakayeomba ufadhili awe amewasilisha maombi kwa njia ya mfumo, awe raia wa Tanzania, mtumishi wa Serikali, awe na barua ya udahili kutoka kwenye chuo kinachotambuliwa na Serikali ndani au nje ya nchi na awe anakwenda kusoma fani za kipaumbele zilizoainishwa na Wizara. Vile vile, ufadhili utazingatia uhitaji unaotokana na uhaba wa taaluma/fani kwenye kituo anachotoka mtaalamu. Kwa mantiki hiyo, kipaumbele cha kupata ufadhili kitategemea upungufu wa taaluma aliyoomba kwenda kusoma kwenye kituo chake cha kazi. Sifa zingine ni kama zilivyoainishwa kwenye tangazo la ufadhili litakalowekwa kwenye tovuti ya Wizara ya Afya.

Wizara ya Afya kwa niaba ya Sekta ya Afya nchini inamshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuipa Sekta hii kipaumbele katika maeneo ya miundombinu, wataalamu wa afya, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Wizara inaahidi kutokumuangusha na na tutafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha kuwa shauku yake ya kuona kila mwananchi anapata huduma za afya zilizo bora na za karibu inatimia.

Asanteni sana.



Jenista J. Mhagama
**WAZIRI WA AFYA**